## Maswali

1. Eliya aliambia Mfalme Ahabu afanye nini?
2. Eliya aliambia watu wajitayarishe kwa kitu gani?
3. Eliya aliambia manabii wa Baali wafanye nini?
4. Manabii wa Baali walifanya nini siku mzima?
5. Baali aliwajibu na kuleta moto?
6. Eliya alifanya nini jioni?
7. Eliya alimwaga mapipa ngapi ya maji juu ya madhabahu?
8. Eliya aliomba nini kwa Mungu?
9. Mungu alijibu maombi yake namna gani?
10. Watu walisema nini walipoona Mungu ametuma moto?
11. Nini ilifanyika kwa manabii 450 wa Baali?

## Majibu

1. Leta watu na manabii 450 wa Baali kwa Mlima wa Karmeli.
2. Kama Baali ni mungu au kama Bwana ni Mungu wa kweli.
3. Jenga madhabahu lakini moto usiwekwe chini yake. Omba Baali atume moto.
4. Waliomba Baali, waliruka ruka juu ya madhabahu na kupiga kelele wakiita.
5. Hapana. Baali hakutuma moto wowote.
6. Eliya alijenga madhabahu kwa mawe 12 na akaweka ndama mme juu yake.
7. Eliya alimwaka mapipa 12 ya maji juu ya madhabahu yake.
8. Eliya aliomba kwamba Mungu aonyeshe watu kwamba Yeye ni Mungu wa kweli.
9. Mungu alituma moto na ulichoma ndama mme, mawe na maji.
10. “Bwana, Yeye ni Mungu.”
11. Manabii wa Baali waliuawa.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1    Mwaka wa 3**

# 31 Eliya kwa Mlima wa Karmeli

## Marejeo

1 Wafalme 18: 1 – 40

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu ni mmoja

## Maneno maalum

31.1 Hakuna mvua + miaka 3 + Mungu + Eliya + Mfalme Ahabu + Mlima wa Karmeli + manabii 450 wa Baali

31.2 Mfalme Ahabu + manabii 450 wa Ahabu + watu + Mlima wa Karmeli + Baali ni mungu wa kweli? + Bwana ni Mungu wa kweli?

31.3 Manabii wa Baali + jenga madhabahu + hakuna moto + omba Baali + lilia Baali + siku mzima + hakuna jibu + hakuna moto

31.4 Jioni + Eliya + jenga madhabahu + hakuna moto + maji mapipa 4 + mara 3 + maji loesha madhabahu + omba Mungu + moto + “Bwana ni Mungu”

31.5 Manabii wa uongo + ua + watu waliabudu Mungu + mvua

**31.1** Haikunyesha kwa miaka mitatu. Mungu alimwambia Eliya aende kwa Ahabu. Mungu aliambia Eliya ambia Mfalme Ahabu kwamba Mungu ataonyesha watu wote kwamba Yeye ni Mungu wa kweli wala si Baali aliye sanamu mwenye watu wanaabudu. Eliya aliambia Mfalme Ahabu alete watu wote juu ya Mlima wa Karmeli na manabii 450 wa Baali.

**31.2** Mfalme Ahabu alituma habari kila mahali kwamba kila mtu aje kwa Mlima wa Karmeli. Muda si muda wote walikusanyika kwa mlima. Eliya na manabii 450 wa Baali walikuwepo pia. Eliya aliambia watu, “Mwamue ni nani ndiye Mungu wa kweli. Kama Bwana ndiye Mungu, basi mwabudu Yeye peke yake. Lakini kama Baali ndiye mungu wa kweli basi mwabudu yeye. Mimi ndimi nabii wa Bwana pekee, lakini kuna manabii 450 wa Baali.”

**31.3** Eliya aliambia manabii wa Baali wajenge madhabahu na waweke juu yake ndama mme lakini wasiwashe chini yake moto. Ni lazima waombe kwa Baali. Kama Baali ni mungu wa kweli, atatuma moto. Manabii wa Baali walitengeneza madhabahu na wakaanza kuomba Baali.

“Ee Baali, tusikie,” waliendelea kuomba, “Baali tunakulilia.” Lakini hakukuwa na jibu. Kwa siku mzima walipiga kelele, “Baali, Baali, tunakulilia. Tusikie na utujibu, Baali. Tusikie na utujibu, Baali, tunakuomba.”

Eliya aliwaangalia. Akawafanyia msaha, “Lia kwa sauti, labda Baali anazungumza, au labda analala mnatakiwa mmuamshe.” Mnabii wa uongo waliendelea kuita kwa sauti, “Baali, Baali, Baali.” Walipiga kelele na kuruka ruka juu ya madhabahu. Lakini hakukuwa na sauti yoyote wala moto haukuwaka kwa madhabahu yao.

**31.4** Mwishowe, kulipokaribia jioni, Eliya aligeuka, akanyoshea watu mikono yake na kuwambia, “Kuja karibu na mimi.” Watu walipokuja karibu naye, Eilya alichukua mawe kumi na mbili na akajengea Mungu madhabahu. Aliweka ndama mme juu ya madhabahu tena akalima mtaro uliouzunguka hayo madhabahu.

Akaita watu fulani na akawambia, “Jaza maji mapipa manne na mumwake juu ya dhabihu.” Manabii wa Baali waliangalia watu wakiteremka haraka chini ya mlima wakienda kuteka maji kwa mapipa manne. “Enda mara ya pili,” Eliya alisema. Walienda kuleta tena. Akawambia waende mara ya tatu, “Enda tena mara ya tatu.” Walienda na kujaza mara ya tatu.

Walipomwaka maji kwa madhabahu, yaliteremka na kuzunguka na kujaza mitaro yenye Eliya alichimba. Kila kitu kwa madhabahu kililoweshwa maji na hata hakukuwa na dalili kwamba viungue chomwa na viungua.



Halafu Eliya aliangalia juu mbinguni. Akaomba, “Bwana Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Israeli. Ijulikane leo kwamba Wewe ni Mungu na mimi ni mtumishi wako. Nisikie mimi, Bwana, nisikie mimi, ili hawa watu wajue kwamba Wewe ni Bwana Mungu wa kweli.”

Kwa ghafula kulikuwa na mwangaza uliomulika na watu wakaogopa. Moto ulitoka juu mbinguni na ukachoma huyo ndama mme na mawe na mavumbi na ikaramba maji yote yaliyokuwa kwa mtaro. Watu waliogopa na kuanguka wakiangalisha nyuzo zao chini. Walisema, “Bwana, Yeye ni Mungu, Bwana, Yeye ni Mungu.”

**31.5** Eliya aliwaangalia manabii wa uongo, waliokuwa wakitoroka. “Shika hawa manabii wa Baali. Musiache hata mmoja atoroke. Waue wote.” Watu waliua manabii wa uongo wote kwa hivyo hakukuwa na kuabudu Baali tena.

Halafu Eliya aliomba kwa Mungu na kukanyesha baada ya muda wa zaidi ya miaka tatu. Kwa hivyo Mungu alionyesha kwamba Yeye ndiye Mungu pekee hakuna mungu mwingine kando yake.